

**MAKAO MAKUU**

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole  
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: [info@ewura.go.tz](mailto:info@ewura.go.tz)

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

## TANGAZO KWA UMMA

### MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJISAFI NA MAJITAKA KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA HTM (HTM WSSA) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

#### Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-019

Mnamo Septemba 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya HTM (HTM WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake kwa kipindi cha 2018/19 - 2020/21. Majedwali namba 1-4 yanaonesha mchanganuo wa bei na ada za sasa zinazopendekezwa.

#### Jedwali 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa za Majisafi (Shilingi/Uniti)

Kundi la Wateja	Matumizi kwa Uniti	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
		2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
	0 -	1,350	86%	2,510	135%	5,910	-31%	4,104
Majumbani	>10	1,360	85%	2,510	135%	5,910	-31%	4,104
	0 -	1,470	87%	2,750	135%	6,475	-31%	4,497
Taasisi	>10	1,490	85%	2,750	135%	6,475	-31%	4,497
	0 -	1,600	86%	2,972	135%	6,997	-31%	4,859
Biashara	>10	1,610	85%	2,972	135%	6,997	-31%	4,859
Viwanda/ Umwagiliaji	0 -	1,860	87%	3,470	135%	8,170	-31%	5,674
	>10	1,880	85%	3,470	135%	8,170	-31%	5,674
	0 -	1,350	86%	2,510	135%	5,910	-31%	4,104
Magati	>10	1,360	85%	2,510	135%	5,910	-31%	4,104
	0 -	900	87%	1,680	135%	3,955	-31%	2,746

Kundi la Wateja	Matumizi kwa Uniti	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
		2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19	Mabadiliko (%)	2019/20	Mabadiliko (%)	2020/21
Maji ya Jumla	>10	910	85%	1,680	135%	3,955	-31%	2,746
Kunyweshea Mifugo	-	910	85%	1,680	135%	3,955	-31%	2,746

**Jedwali 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuunganishiwa Huduma ya Majisafi - Shilingi/Maunganisho**

Kundi ka Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa		
	2017/18	2018/19	2017/18	2018/19
Wateja wote	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na wafanyakazi	Asilimia 20 ya gharama za vifaa na wafanyakazi		

**Jedwali 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Majisafi – Shilingi/Kurejeshewa Huduma**

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa Asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa Asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa Asilimia	2020/21
Majumbani	11,000	355%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Taaasisi	14,000	257%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Biashara	15,000	233%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Viwanda/ Umwagiliaji	20,000	150%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Magati	11,000	355%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Maji ya Jumla	20,000	150%	50,000	0%	50,000	0%	50,000
Kunyweshea Mifugo	20,000	150%	50,000	0%	50,000	0%	50,000

**Jedwali 4: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)**

Kundi La Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Inayopendekezwa			
	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	
Wateja Wote	1,500	0	0	0	

Kutokana na HTM WSSA, sababu za mabadiliko ya bei ni pamoja na kuongezeka kwa gharama za pembejeo katika soko na kutakiwa kulipa gharama zote za umeme wa kuzalisha maji ambayo hapo awali ikilipwa na Wizara ya Maji. Mapitio ya bei yatasababisha huduma ya majisafi kuwa bora na endelevu. Pia, mapitio ya bei yatahakikishia utekelezaji wa Mpango Biashara na kufikiwa kwa malengo ambayo yamelenga kutoa huduma bora ya majisafi kwa wakazi wa Handeni na baadhi ya vijiji vya Korogwe.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano

wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 24 Januari 2019 katika ukumbi wa CCM uliopo wilayani Handeni** kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa HTM WSSA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu **ifikapo tarehe 28 Januari 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika **OFISI ZA EWURA KANDA YA KASKAZINI, GHOROFA YA PILI, JENGO LA PPF PLAZA; LINALOFUATANA NA HOTELI YA KIBO PALACE, ENEO LA CORRIDOR au OFISI ZA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA HANDENI TRUNK MAIN ZILIZOPO MJINI KOROGWE.**

**Imetolewa na:**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)**

**3 Januari 2019**